



# Hapa usalama tu?

## Usalama, polisi na haki nchini Tanzania

### 1. Utangulizi

Jukumu la kwanza la serikali ni kuwalinda wananchi wake na Jeshi la Polisi lina dhamana kuu katika utekelezaji wa jukumu hilo nyeti. Vile vile, katika miaka ya hivi karibuni polisi jamii, maarufu kama sungusungu, wamefanya kazi kubwa ya kulisaidia Jeshi la Polisi katika kuhakikisha jamii za kitanzania ziko salama.

Kumekuwepo na mfululizo wa matukio ya mauaji yanayotishia hali ya Usalama nchini Tanzania hususani yanayotokea Kibiti, Mkoani Pwani. Matukio haya yamekuwa yakiripotiwa sana katika vyombo habari na kusababisha hofu kutanda nchini. Lakini tukumbuke kwamba matukio haya siyo kiashiria rasmi cha hali ya usalama nchini kote. Ni muhimu kupata mitazamo ya wananchi ili kuelewa hali halisi walionayo wao. Mitazamo ya umma ni moja ya vyanzo vikuu muhimu vya ushahidi kuhusu hali ya usalama kwa ujumla; japokuwa mitazamo hiyo huweza kuwa imechangiwa na vyombo vya habari na uwepo wa taarifa

finyu juu ya matokeo ya uhalifu nchini. Kwa vile mitazamo ya umma ndio kiini cha uundaji wa sheria na taratibu, basi hatuna budi kuyazingatia.

Muhtasari huu umebeba takwimu kuhusu maoni ya wananchi juu ya usalama, polisi na haki nchini Tanzania. Ni kwa kiasi gani wananchi wanajisikia wapo salama kwenye nyumba zao na katika maeneo wanayoishi? Wanachi wana uzoefu gani kuhusu uhalifu? Jeshi la polisi lina jukumu gani katika kuhakikisha ulinzi na usalama? Viongozi wa serikali za mitaa na sungusungu wana jukumu gani? Ni kwa kiwango gani wananchi wana imani na uwezo wa mifumo ya utoaji haki katika kuwaadhibu wananchi na watu maarufu wanaofanya uhalifu?

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* ambao huratibiwa na taasisi ya Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni

utafiti wenyewe uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi; na wenyewe uwakilishi wa Tanzania Bara pekee. Zanzibar haihusiki kwenye utafiti huu. Takwimu za muhtasari huu, zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,805 katika awamu ya 18 ya kundi la pili la Sauti za Wananchi. Takwimu hizi zilikusanywa kati ya Machi 31 na Aprili 17, 2017. Kwa maelezo zaidi kuhusu namna utafiti *Sauti za Wananchi* unavyoratibiwa tafadhali tembelea [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti)

Inapaswa kufahamika kuwa kundi la wahojiwa wa *Sauti za Wananchi* hupatikana kutoka maeneo mia mbili (200) yaliyochaguliwa kinasibu kutoka Tanzania Bara. Kila eneo huwakilishwa na wahojiwa kadhaa. Hivyo, katika maswali yanayohusiana na maeneo au jamii za wahojiwa, mwingiliano huweza hutokea kutoptaka na mhojiwa zaidi ya mmoja kutoa majibu yanayohusiana na kila eneo. Hii husababisha upungufu kidogo katika uwakilishi wa Tanzania Bara hususani kwenye maswali yahusuyo maeneo. Lakini katika maswali yahusuyo kaya na watu binafsi, uhakika wa uwakilishi wa Tanzania Bara unabaki palepale.

Matokeo muhimu ni:


- Wananchi sita kati ya kumi wanadamu wizi ni tishio kubwa la usalama katika maeneo wanayoishi.
- Nusu ya wananchi wanademu usalama kwenye maeneo yao umeimarika katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.
- Wananchi wawili kati ya watatu wanademu wanaomba msaada kutoka kwa viongozi wa vijiji au mitaa linapotoka tukio la uhalifu.
- Karibu nusu ya wananchi wanaishi kwenye kijiji/mtaa usiokuwa na kituo cha polisi.
- Mwananchi mmoja kati ya wawili wanaridhika na huduma zinazotolewa na polisi.
- Wananchi wanane kati ya kumi wana sungusungu kwenye maeneo wanayoishi.
- Wananchi wawili kati ya watatu wanademu wananchi wa kawaida mara zote au mara nydingi huadhibiwa kwa mujibu wa sheria wakati wananchi watatu kati ya wanane wanademu matajiri huadhibiwa mara chache ama hawaadhibiwi kabisa.

## 2. Mambo nane kuhusu maoni ya wananchi kuhusu usalama na polisi

### Jambo la 1: Wananchi 6 kati ya 10 wanademu wizi ni tishio kubwa la usalama katika maeneo wanayoishi

Asilimia 61 ya wananchi wanademu wizi ni tishio kubwa kwa usalama katika maeneo wanayoishi. Masuala mengine yaliyoanishwa ni wizi wa mifugo (asilimia 5), vikundi vyya wahuni (asilimia 3), vijana wasio na ajira (asilimia 3), watumiaji wa dawa za kulevya (asilimia 2) na wachawi (asilimia 2).


## Kielelezo cha 1: Nini tishio kubwa la usalama katika jamii yako?



**Chanzo cha takwimu:** Ufafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Mwananchi mmoja kati ya wanne (asilimia 27) alibibi fedha ama kitu cha thamani katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyopita. Wananchi wawili kati ya watano hawajawahi kuibowi.

## Kielelezo cha 2: Lini mara ya mwisho uliibiwa pesa/kitu cha thamani?



**Chanzo cha Takwimu:** Ufafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Hakuna mabadiliko makubwa katika idadi ya watu walioobiwa kati ya mwaka 2013, 2015 na 2017 (haijaoneshwa kwenye jedwali).

## Jambo la 2: Idadi kubwa ya wananchi wanasema kiwango cha usalama kimeimarika kwenye maeneo yao katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita

Kuna mtazamo wa jumla mionganii mwa wananchi kuwa usalama nchini umeimarika katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita kama inavyooneshwa na zaidi ya nusu ya wananchi hao (asilimia 53). Lakini mwananchi mmoja kati ya kumi (asilimia 10) anaona kuwa usalama umepungua katika kipindi hicho hicho.

## Kielelezo cha 3: Katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, je, unadhani kiwango cha usalama katika jamii yako kime...?




**Chanzo cha Takwimu:** Ufafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Asilimia 29 ya wananchi hawakujisikia salama walipokuwa katika maeneo yao na asilimia 26 katika nyumba zao angalau mara moja katika kipindi cha huu mwaka mmoja uliopita. Asilimia 16

walikaa nyumbani angalau mara moja mwaka jana kutokana na hofu ya vurugu nje ya nyumba zao.


#### Kielelezo cha 4: Mwaka uliopita, mara ngapi ...



**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Takwimu za *Sauti za Wananchi* zinaonesha ongezeko la watu wanaosema hawajawahi kujisikia hawako salama katika maeneo wanayoishi (2013: asilimia 55, 2017: asilimia 71) huku wanaosema hawajisikii salama muda wote wakipungua (2013: asilimia 18, 2017: asilimia 5)

#### Kielelezo cha 5: Mwaka uliopita, mara ngapi, kama iliwahi kutokea, ulijisikia hauko salama kutembea katika eneo unaloishi?




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

#### Jambo la 3: Wananchi wanne kati ya kumi wameshuhudia vurugu hadharani mwaka uliopita

Asilimia 41 wameshuhudia vurugu zikitokea hadharani katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, lakini asilimia 3 tu ndio waliokuwa waathirika wa vurugu hizo.

### Kielelezo cha 6: Lini mara ya mwisho uli...



■ Ndani ya miezi 6 ■ Miezi 7 hadi 12 iliyopita ■ Zaidi ya mwaka mmoja uliopita ■ Sijawahi/sina uhakika

**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017


Miongoni mwa waliokuwa waathirika wa vurugu (wahojiwa 75), asilimia 40 walipigwa, asilimia 18 walifanyiwa vitendo vya kikatili na asilimia 17 walinyang'anya ardhi yao (haijaoneshwa kwenye jedwali).

### Jambo la 4: Wananchi wawili kati ya watatu hutafuta msaada kwanza kwa viongozi wa vijiji au mitaa wakati wa tukio la uhalifu

Pindi wanapokumbwa na tukio la uhalifu, asilimia 66 hutafuta msaada kwa mwenyekiti wa kijiji/mtaa, ukilinganisha na asilimia 26 ambao huenda kwanza polisi.

Wananchi wa vijijini (asilimia 72), wana uwezekano mkubwa zaidi wa kwenda kwa wenyeviti wa vijiji na mitaa kuomba msaada kuliko wananchi wa mijini (asilimia 54). Vile vile, wananchi masikini (asilimia 76) pia huona ni uamuza mzuri zaidi kuwatemebelea wenyeviti wa vijiji na mitaa kwanza kuliko wananchi matajiri (asilimia 50) wenye mtazamo huo huo. Japokuwa matajiri wana uwezekano mkubwa wa kuomba msaada polisi (asilimia 42), wengi wao hupendelea kwenda kwa mwenyekiti wa kijiji ama mtaa (asilimia 50).

### Kielelezo cha 7: Kama ukiwa muathirika wa uhalifu, nani, kama yupo, utaenda kwake kwanza kuomba msaada?



■ Mwenyekiti wa kijiji/mtaa ■ Polisi ■ Familia / marafiki ■ Wengine

**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Asilimia 56 wanasema wanatoa taarifa ya wizi kwa mamlaka pindi wanaposhambuliwa wao wenyewe ama nyumba zao. Asilimia 58 wanasema uhalifu kama huo huwa unaripotiwa mara zote unapotokea kwenye maeneo wanayoishi. Hata hivyo, asilimia 21 wanasema hawatoi taarifa za uhalifu kuhusu wao wala kaya zao na asilimia 8 wanasema uhalifu huo ukitokea katika jamii anayoishi, hauripotiwi.

#### Kielelezo cha 8: Kutoa taarifa ya uhalifu




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Wananchi walipoulizwa ni kwa nini baadhi ya watu hawatoi taarifa za uhalifu kwa polisi, majibu yalitofautiana. Wengine walitaja hofu ya wahalifu kulipiza kisasi (asilimia 16), kukosekana kwa polisi katika eneo lao (asilimia 16), uhalifu kuripotiwa kwenye mamlaka nyingine (asilimia 16), polisi kutowasikiliza ama kutowajali wananchi (asilimia 12), au polisi kuomba pesa/rushwa ili watoe msaada (10%) (haijaoneshwa kwenye jedwali).

#### Jambo la 5: Wananchi wawili kati ya watatu hawana kituo cha polisi dakika 30 kutoka nyumbani kwao

Asilimia 55 ya wananchi wa mjini wana vituo vya polisi ndani ya mwendo wa dakika 30 kutoka eneo wanaloishi, ukilinganisha na asilimia 23 maeneo ya vijijini. Kwa ujumla, mwananchi mmoja kati ya watatu wanaishi mbali ndani ya mwendo wa dakika 30 kufika kilipo kituo cha polisi cha karibu.

#### Kielelezo cha 9: Unachukua muda gani kufika katika kituo cha polisi cha karibu?



**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017


Inawezekana kwamba wananchi wengi wanaona ni bora kutafuta msaada kutoka kwa mwenyekiti wao kwanza kwa sababu vituo vingi vya polisi viro mbali au katika maeneo mengine ni vichache.

Asilimia 32 ya wananchi wana kituo cha polisi kwenye vijiji na mitaa yao, na asilimia 25 wana kituo katika kata zao. Maana yake ni kwamba asilimia 43 hawana kituo cha polisi kwenye kata zao.

Sera ya serikali haina mkakati wa kuwa na kituo cha polisi kwenye kila kata, lakini hulenga kuwa na angalau kituo kimoja kwa kila tarafa.<sup>2</sup>

Katika suala hili hili, utofauti unaonekana kati ya maeneo ya vijijini na mijini: wakazi watatu kati ya wanenye wa maeneo ya mijini (asilimia 73) wana kituo cha polisi kwenye kata zao, ukilinganisha na nusu (asilimia 50) ya maeneo ya vijijini.


#### **Kielelezo cha 10: Je, una kituo cha polisi kwenye kijiji/mtaa, au kata yako?**



**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Linapokuja suala la namba za dharura za polisi na zima moto, kiwango cha ufahamu wa namba hizi ni mdogo sana. Ni asilimia 4 pekee wanaofahamu namba za simu za polisi, na asilimia 1 tu wanaofahamu namba za zima moto. Wengine walifikiri wanafahamu namba hizo, lakini walipoombwa wazitaje, walizikosea.

#### **Kielelezo cha 11: Taja namba ya dharura ya polisi na zima moto?**



**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017


#### **Jambo la 6: Nusu ya wananchi wanaridhika na huduma zinazotolewa na polisi, nusu yao hawaridhiki**

Asilimia 47 wanaripoti kuridhishwa na huduma zinazotolewa na jeshi la polisi, huku asilimia 27 wakiripoti kutokuridhishwa nazo. Uhusiano mdogo sana unaonekana kati ya ukaribu wa vituo vya polisi na kuridhika kwa wananchi na huduma za polisi. Mionganini mwa walio na kituo cha polisi

<sup>2</sup> [https://tanzania.go.tz/egov\\_uploads/documents/MAMBO-NDANI\\_sw.pdf](https://tanzania.go.tz/egov_uploads/documents/MAMBO-NDANI_sw.pdf)

kwenye kijiji/mtaa wao, asilimia 51 wanaridhika na huduma, ukilinganisha na asilimia 44 ya wale wasiokuwa na kituo cha polisi maeneo ya karibu.


#### **Kielelezo cha 12: Ni kwa kiwango gani unaridhika na huduma zinazotolewa na jeshi la polisi?**



**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Sababu kubwa iliyotolewa ya kuridhika na utendaji kazi wa polisi ni kuwa wanasaidia kuzuia uhalifu (asilimia 12 - ya wananchi wote), kutatua uhalifu (asilimia 9) au kwa kuwa wanajali wananchi (asilimia 9). Sababu kuu ya kutoridhishwa na utendaji kazi wa polisi ni vitendo vya rushwa (asilimia 10) kuchelewa kwao katika kutoa msaada (asilimia 4) na utendaji duni wa kazi (asilimia 2).

#### **Kielelezo cha 13: Kwanini unaridhika/hauridhiki na utendaji wa polisi?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

#### **Jambo la 7: Wananchi wanne kati ya kumi wana sungusungu kwenye maeneo wanayoishi**

Asilimia 39 ya wananchi wana vijana wanaojitolea kulinda (sungusungu) katika maeneo wanayoishi. Vikundi hivi ni maarufu zaidi maeneo ya vijijini (asilimia 42) kuliko mijini (asilimia 32) – labda kwa sababu ya uwepo wa vituo vichache vya polisi kwenye maeneo hayo.

### Kielelezo cha 14: Je, kuna sungusungu katika eneo unaloishi?




**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Miongoni mwa wale wenye sungusungu katika maeneo wanayoishi, idadi kubwa (asilimia 78) wanaridhika na huduma inayotolewa. Ni asilimia ndogo tu (asilimia 7) isiyoridhishwa.

### Kielelezo cha 15: Ni kwa kiasi gani unaridhika na huduma zinazotolewa na sungusungu kwenye jamii yako?

(miongoni mwa wale wenye sungusungu; n=685)



**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Asilimia 88 ya wananchi wote wanakubali kuwa sungusungu ni muhimu kwa kuwa wanalinda usalama. Miongoni mwa mwenye sungusungu, asilimia 78 wanasema kiwango cha usalama kimeimarika tangu vikundi vya sungusungu vilipoanza kufanya kazi (haijaoneshwa kwenye jedwali).

Hata hivyo, wananchi wengi wanaonekana kuwa na imani zaidi na polisi (asilimia 59) katika kuwalinda kuliko sungusungu (asilimia 41).

### Kielelezo cha 16: Imani ya wananchi kwa polisi na sungusungu katika kuwalinda: (chagua kauli ambayo unakubaliana nayo zaidi)



**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Hata hivyo, walipouliwa namna nzuri ya kupunguza uhalifu unaotokea nyakati za usiku, wananchi wengi waliunga mkono uundaji wa vikundi vya sungusungu (asilimia 47) kuliko kushauri kuongeza doria za polisi (asilimia 44) (haijaoneshwa kwenye jedwali).


## Jambo la 8: Wananchi 2 kati ya 3 wanasema watu wenye 'nguvu' wapo juu ya sheria

Asilimia 65 ya wananchi wanasema wanapoiba ama kufanya uhalifu wowote, mara zote huadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Hii imepanda kutoka asilimia 48 waliosema hivyo hivyo mwaka 2013.

Hata hivyo, idadi kubwa ya wananchi wanasema watumishi wa umma (asilimia 68), viongozi wa dini (asilimia 68) maofisa wa polisi (asilimia 69), viongozi waandamizi wa serikali (asilimia 72) na watu matajiri (asilimia 74) huadhibiwa mara chache sana, ama hawaadhibiwi kabisa, pale wanapofanya uhalifu.

Imani ya wananchi kwa mfumo wa utoaji wa haki kuwaadhibu watu wenye uwezo, maarufu, au wenye ushawishi katika jamii umeongezeka tangu mwaka 2015, lakini umebakia kuwa chini kuliko ilivyokuwa mwaka 2013.

**Kielelezo cha 17: Ni mara ngapi unadhani kuwa watu wafuatao wakiiba ama kufanya uhalifu hapa nchini Tanzania, watawajibishwa kwa mujibu wa sheria?**




■ Mara chache/sidhani   ■ Mara zote/mara nyingi

**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 18 - Aprili 2017

Wananchi wenyewe uwezo (asilimia 15) hawafikiri kwamba kuna uwezekano wa watu matajiri kuadhibiwa kwa makosa waliyofanya. Hata hivyo, asilimia 32 ya watu maskini sana wanafikiri kuwa matajiri wataadhibiwa ipasavyo.

#### **Kielelezo cha 18: Unafikiri kuwa mtu tajiri akiiba ama akifanya uhalifu hapa Tanzania, ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria? (kwa kiwango cha hali za kiuchumi za wahojiwa)**



**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 - Aprili 2017

### **3. Hitimisho**

Muhtasari huu una habari njema. Wananchi wengi wanasema hali ya usalama kwenye maeneo yao imeimarika katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Lakini idadi sawa na hiyo bado wanasema hali si shwari. Wananchi wengi wanasema wamekuwa wakijisikia salama wakati wanapotembea katika maeneo wanayoishi mwaka 2017 kuliko iliyokuwa mwaka 2013 au 2015. Mara mbili zaidi ya wananchi wanaridhishwa na utendaji wa polisi. Na sehemu zenye sungusungu, wananchi huridhishwa na huduma zao. Hizi zote ni dalili muhimu – japokuwa vichwa vyatya habari vimetawaliwa na matatizo makubwa ya kiusalama katika wilaya ya Rufiji.

Itakuwa ni kosa kuhitimisha kuwa kuwa hali ni shwari kabisa. Mwananchi mmoja kati ya wanne aliibiwa fedha ama kitu kingine cha thamani mwaka uliopita, na wananchi watatu kati ya kumi hawakujisikia salama wakitembea katika maeneo yao katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Ni idadi inayopaswa kuangaliwa.

Bado kuna tatizo katika suala la imani walijonayo wananchi kwa polisi. Kwanza, asilimia 43 hawana vituo vya polisi kwenye vijji/mitaa ama katika kata zao, na hii huonekana zaidi katika maeneo ya vijijini (asilimia 50). Ni asilimia 26 pekee wanaosema endapo watakuwa waathirika wa vitendo vya uhalifu watatafuta msaada kwanza polisi, ukilinganisha na asilimia 66 ambao watatafuta msaada kwanza kutoka kwa mwenyekiti wa kijiji/mtaa.

Hii inaonesha kuwa wananchi hawaoni kama polisi ni kimbilio lao la karibu na lenye uwezo wa kutoa msaada pindi uhalifu unapotokea. Hitimisho hili hutokana na wananchi kuonesha kuridhishwa au kutoridhiswa kwao na polisi bila kujali ukaribu wao na vituo vya polisi. Kwa kufafanua zaidi, tumeona kuwa uwepo wa kituo cha polisi karibu na wananchi huchangia

wananchi kutoa taarifa polisi pindi uhalifu unapotokea. Lakini ukaribu wa polisi haukubadilisha mtazamo wa wananchi juu ya huduma zao. Vitendo vya polisi kuongoza katika kuvunja haki za binadamu nchini vimeripotiwa sana; ni vizuri kuangalia ni aina gani ya huduma ambazo wananchi wengi wanatarijia kutoka kwa polisi.

Sungusungu kwa kawaida huanzishwa kwa kibali rasmi kutoka serikali za mitaa na polisi wa eneo husika. Baadhi ya wahojija wanaona sungusungu kama mbadala wa polisi pale ambapo polisi wanashindwa kufikia kila jamii wakati wote. Muhtasari huu unaonesha kuwa wananchi wengi wanaunga mkono ulinzi wa sungusungu. Lakini ni wananchi wanne tu kati ya kumi wenye sungusungu kwenye jamii zao. Na mahali ambapo sungusungu hao wapo, asilimia 78 wanaridhishwa na huduma wanazozitoa. Wakati wananchi wengi zaidi wanasema wana imani zaidi na polisi kuliko sungusungu, asilimia 88 wanakubali kuwa sungusungu ni muhimu kwa vile husaidia kuhakikisha usalama, na asilimia 78 ya wenye sungusungu wanasema kiwango cha usalama kimeimarika tangu sungusungu walipoanza kazi. Zaidi, walipoulizwa namna nzuri ya kupunguza uhalifu unaotokea usiku, wananchi wanasema ni kwa kuongeza vikundi vya sungusungu (asilimia 47) kuliko wanaoshauri kuongezwa kwa doria za polisi (asilimia 44).

Suala lingine la kuzingatia ni mitazamo ya wananchi kuwa watu wenye nyadhifa na mamlaka, wakiwemo watumishi wa umma, viongozi wa dini na watu matajiri; wanaonekana kutowajibika kwa makosa wanayofanya. Kati ya robo na theluthi ya wananchi wanaona kuwa watu hao wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria kama watafanya makosa. Lakini zaidi ya asilimia 50 ya wananchi wanaona kuwa wananchi wa kawaida na wa hali ya chini ndio wataadhibiwa ipasavyo pindi wafanyapo makosa.

Kwa ujumla ujumbe unaopatikana hapa ni kwamba wakati uzoefu wa wananchi wengi ukionesha kuwa hali ya usalama inaimarika, hatupaswi kuridhika. Japokuwa vikundi vya sungusungu vinaweza kuziba pengo la polisi, isiwe ndiyo kigezo cha polisi kukwepa majukumu yao. Kuna mambo mengi ya kunufaisha umma endapo polisi watafanya jitihada za dhati za kukaa karibu zaidi na wananchi. Masuala mawili muhimu zaidi kwa polisi kwanza ni kusogea karibu na wananchi kwa kuanzisha vituo vingi zaidi vya polisi, na pili kujenga uaminifu na imani kwa wananchi.